OFI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

Simu: 0787 886 610 (H/M)
0767 941 425 (H/M)
0682324009 (S/M)

Email: mulbadaw@hanangdc.go.tz

SHULE YA SEKONDARI MULBADAW,
S. L. P 141,
25-04-2024
KATESH- HANANG.

Unapojibu tafadhali taja:-
Kumb. Na. MSS/ADM/J.INSTR. FV/VOL.I/01/2024

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI…………………………………………….
S.L.P ……………

**YAH: MAELEEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MULBADAW KIDATO CHA TANO JULAI 2024/2025 WILAYA YA HANANG, MANYARA.**

***UTANGULIZI***

Nafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari MULBADAW kwa mwaka 2024 katika tahasusi ya CBG,PCB au CBA.

Shule ya sekondari Mulbadaw iko umbali wa Km 30 Kaskazini-Magharibi mwa mji wa Katesh ambapo ndio makao makuu ya Wilaya ya Hanang. Usafiri wa magari kutoka Katesh kuja shuleni Mulbadaw unapatikana kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi 12:30 jioni standi ya Katesh kwa Magari yanayoelekea Hydom na nauli ni shilingi 4,000/= mpaka shuleni (kituo cha kushukia kinaitwa CMSC, au unaweza kushuka kona ya Sekondari Mulbadaw).

Aidha, wanafunzi wote wa kidato cha tano 2024 wanatakiwa kuripoti shuleni kuanzia 01/07/2024 kwa ajili ya kupewa maelekezo muhimu ya kozi yao (orientation course) .
MUHULA WA MASOMO UTAANZA TAREHE 14/07/2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 13/07/2024 saa 10:00 jioni.

Hongera na karibu sana Shule ya Sekondari Mulbadaw.

________________________

**MKUU WA SHULE**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1. MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE**

1. Bima ya Afya kwa mwaka ni Tsh. ………………………………………..50.400/= Au aje na kitamburisho cha bima ya Afya NHIF na sio ICHF kama anacho

**2. Michango mingine muhimu.**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B.** Malipo yote yanapaswa kufanyika katika Benki ya **NMB** kwa Akaunti Ifuatayo:- Shule ya sekondari Mulbadaw **A/C.No. 41001200061**. Unapaswa kuleta **Original Bank pay in slip** inayoonesha jina la mwanafunzi, na aina ya malipo **mfano:-** Bima ni Tsh 50,400/= Tahadhari ni Tsh 5,000/=n.k

***(Hatutapokea fedha taslimu).***

**1:2. VIFAA VYA DARASANI.**

**1.** Daftari kubwa 'counter book'' 10 au zaidi
**2.** Kalamu za wino na penseli.
**3.** Rula na kifutio.
**4.** Karatasi za photocopy (Ream 1 (A4) kwa muhula.
**5.** Picha mbili (2) passport size za rangi za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu.
**6.** Scientific calculator kwa mwanafunzi, ambazo ni 'Non- programmable'
**7.** Dissecting kit **lazima Kwa wanafunzi wanaosoma Biology**

**8. VITABU**: Vitabu ni muhimu sana kwa mwanafunzi kwani humpatia maarifa kamili juu ya masomo yake mbalimbali kwa wakati husika. Shule ina vitabu vichache sana, na itaendelea kununua vitabu kulingana na kasma itolewayo na serikali kwa kifungu hicho. Kila mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mtoto wake angalau nakala chache za vitabu kulingana na Tahasusi ya mwan

**VIFAA VYA USAFI NA VYOMBO VYA CHAKULA.**

- Ndoo 2 za plastic za lita10.
- Toilet brush (mabrashi ya kusafisha vyoo -mafupi)
- Drying mopper (squeezer) ya kudekia.
- Jembe moja(1)
- Reki moja(1).
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

**SARE YA SHULE:**

Mzazi hakikisha mwanao ana:-

(i) Sketi mbili za kitambaa kizito rangi ya dark bluu (Zenye mshono wa rinda box toka juu hadi chini mbele na nyuma na kulia na kushoto marinda madogo ya kawaida ) ziwe ndefu inch 8 baada ya magoti

(ii) Suluali pea mbili kitambaa kizito rangi ya dark bluu zenye linda mbili na mkunjo kwa chini ( Mnyonyo na suluali za kubana haziruhusiwi)

(iii) Mashati meupe mawili ya mikono mirefu (tetron), wavulana na wasichana. Aidha, kwa wasichana wa kiislamu watavaa nusu kanzu na kitambaa cha kichwani cheupe chenye kufunika masikio na mabega (ushungi) usiwe na urembo – asinunue tai.

(iv) Tai moja (1) rangi ya sketi/suluali na pini moja.
(v) Sweta dark blue lenye V.shape mbele.
(vi) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufungua kamba na vyenye visigino vifupi.
(vii) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe kwa wasichana na rangi ya khaki kwa wavulana.
(viii) T - Shirt pana, damu ya mzee (isiyo na maandishi).
(ix) Shamba dress kwa wasichana sketi 1 kitambaa kizito rangi ya kahawia (brown) ya marinda ya kawaida ziwe ndefu na wavulana suluali 1 kitambaa kizito rangi ya kahawia.
(x) Raba za michezo (zenye kamba) rangi yoyote na soksi ndefu rangi ya blue (stockings).
(xi) Bukta na T-shirt (Jezi) ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo.
(xii) Tracksuit rangi nyeusi.
(xiii) Suruali nyeusi isiyobana na isiyo ‘transparent’ kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa kujisomea

**Matandiko. (Ujinunulie)**
xiv) Mashuka ya rangi ya light blue iliyoiva na pink iliyokolea na foronya zake. xv) Mto (1)
xvi) Taulo
xvii) Kitenge au kanga 2 kwa ajili ya kuogea kwa wasichana. xviii) Neti nyeupe Square ‘4 x4’
xix) Godoro lenye ‘cover’ ‘2½ x6’
xx) Blanket moja.

**1.3 SHERIA ZA SHULE.**
**A: HESHIMA.**
1) Wanafunzi wawe na heshima kwa waalimu, Wafanyakazi wote wa shule, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote anayewazidi kwa umri.
2) Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote wenyewe kwa wenyewe, kwa waalimu na watu wengine.
3) Wanafunzi wote hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo;
a) Kuvuta sigara, bangi na kutumia madawa ya kulevya kama mirungi mihadarati nk. b) Kunywa pombe za aina yoyote.
c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama kofia, nguo fupi zakubana.
d) Kugombana. e) Kufuga ndevu
f) Kufuga kucha na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
g) Kunyoa kipara.
h) Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi yatafanyika kupitia simu ya shule.
I) Kusuka nywele hairuhusiwi kabisa.
4) Wanafunzi wote ni lazima washirikiane na kusaidiana na waheshimu na wathamini kazi za aina zote zilizo halali.
5) Wanafunzi watatakiwa kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mwalimu au kiongozi anayewaita, marawaitwapo.
6) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha ya viongozi wa serikali wimbo wa Taifa, na fedha zaTaifa.
7) Wanafunzi waheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule kutunza na kuthamini mali ya binafsi na mali ya umma
8) Wanafunzi wawe mfano mzuri wa heshima mahali popote watakapokuwa.
9) Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
10) Wanafunzi wanyooshe mikono juu na wasimame wanapouliza na kujibuswali.
11) Uhusiano kati ya wavulana na wasichana uwe wa kimasomo tu.
12) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba wimbo waTaifa na nyimbo nyingine za kizalendo.

**B: MAHUDHURIO.**
i) Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote vya masomo nje na ndani yadarasa. ii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie kazi zote za mikono
iii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa n.k.
iv) Wanafunzi watakaopangwa zamu wakati wa likizo lazima wahudhurie zamu bila kukosa.
**C: KUWAHI.**
i) Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa kurudi shule baada ya likizo,n.k.
i) Wanafunzi ni lazima kuwahi haraka wanaposikia wito wa dharura au kengele.

**D: SARE ZA SHULE.**

Ni lazima wanafunzi wote wavae sare za shule wakati wote wa:

a) Masomo ya darasani.
b) Wanapotoka nje kwa shughuli za shule.
c) Mhadhara wa shule (Baraza).
d) Wanapokwenda hospitalini.
e) Maandamano rasmi.
f) Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo yoyote hayaruhusiwi kuvaliwa na sare za shule.
g) Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa shuleni lazima uzingatiwe kwa kilahali.
h) Wanafunzi wawe na kitambulisho na nembo ya shule kwenye mfuko wa shati la shule.

**E: MIPAKA YA SHULE.**

1. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya kibali / ruhusa ya maandishi na warudi kwa saa zilizoruhusiwa/pangwa.

2.Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ya kibali cha maandishi cha mwalimu.

i) Ofisi zashule.
ii) Nyumba za waalimu na wafanyakazi wasio waalimu.
iii) Vilabu vya pombe.
iv) Nyumba za starehe
v) Nyumba za kufikia wageni.

**NB.** (iii), (iv) na (v) hakuna ruhusa/ kibali kinachotolewa.

**F: USAFI.**

Kila mwanafunzi lazima azingatie usafi wa vifaa vyote wanavyotumia hapa shuleni na usafi wake binafsi (wa mwili)

Kila mwanafunzi ni lazima awajibike kwa usafi wa mazingira ya shule. Ni marufuku kutupa karatasi ovyo, na ni marufuku kupita njia za vichochoro, kila mwanafunzi lazima atunze bustani za maua kwa kilahali.

**1.4. MAKOSA YATAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba ndani au nje ya Shule.
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia kifaa cha mawasiliano/simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau Bendera yaTaifa.
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali yoyote ya umma kwa makusudi

**MUHIMU (TANBIHI).**

Adhabu kwa uvunjaji wa sheria za shule zitatolewa na Mwalimu wa Nidhamu, Baraza la Waalimu, Bodi ya Shule au vyombo vingine vinavyohusika.

Kila mwanafunzi aje na cheti halisi cha kuzaliwa na Kivuli chake (Photocopy) pamoja na hati ya matokeo (result slip).

5 **ANGALIZO**.

Siku ya kufungua shule zoezi la ukaguzi litafanyika kikamilifu. Mwanafunzi ambaye atashindwa kutimiza mahitaji yote muhimu hatapokelewa.

**NB**: Wanafunzi hawaruhusiwi; Kuja au kuletewa simu ya aina yoyote shuleni.

i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja na wala kuletewa aina yoyoye ya chakula shuleni.
ii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na manukato wala vipodozi shuleni.

**MWISHO**: Ni matarajio yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii ya pekee uliyopewa na serikali na utakuwa mfano mzuri wa **KITAALUMA, NIDHAMU, KAZI, USAFI, NA MICHEZO**.

Nakutakia
mafanikio mema

________________________

**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATISHO B**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI.**

**SHULE YA SEKONDARI MULBADAW S.L.P 141,**

**HANANG-MANYARA**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE PAMOJA NA MASHARTI YAKE MWAKA 2024.**

**A: MWANAFUNZI.**

Mimi..................................................nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari MULBADAW. Pia nimesoma na kuelewa vema sheria za shule, Kwa heshima na taadhima ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu zifuatazo:- (Iwapo unakubali nafasi hii toa sababu vivyo hivyo kama unakataa nafasi hii toa sababu).

.........................................................................................................................................

.........................................................................................

Tarehe.......................................................Saini.............................

**B: MZAZI/MLEZI** Mimi......................................................Mzazi/mlezi wa ...........................

Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mulbadaw .Nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo,ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza,kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi,wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa eleza sababu.

...................................................................................................................................

..........................................................

Ahsante.

(i)Jina la mzazi/mlezi....................................................

Anwani...................................................

Namba ya simu ya mkononi....................................

Tarehe....................................Saini...............................

Ndugu/jamaa (3) watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mototo/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.

N.B Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzi.

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu/jamaa wa karibu ambao wanaoweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo.

Jina la mzazi/mlezi.............................................................Saini.............................

| S/N | MAJINA MATATU | UHUSIANO WAKE NA MTOTO | ANWANI | SIMU YA MKONONI | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |

***Kata lisilohusika**

**N.B Sehemu ‘B’ijazwe na kusainiwa na mzazi na si vinginevyo**

**ATTACHMENT B.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

MULBADAW SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 344,
HANANG– MANYARA.
25-05-2024

Ref.No. MSS/ADM/J.INS. FV/VOL. 1/01/2024
TO THE MEDICAL OFFICER.
.....................................................
....................................................(GOVERNMENT HOSPITAL)

STUDEN'S NAME..............................................................AGE.................YEAR...................... ..

Please examine the above named student and arrage for any necessary treatment for student if need be.

**Sinkamba, C.M**

THE HEAD MASTER. MEDICAL
CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)

I have examined the above named with regard to:

REMARKS. SKIN...............................................................................................
EYES............................................................................................
EARS.............................................................................................
TEETH.........................................................................................................
B/S TEST (CHRONIC)..............................................................................
PRESSURE...........................................................................................
ABDOMEN..........................................................................................
CHEST...............................................................................................
STOMACH..........................................................................................
URINE.................................................................................................
H.B HAEMOGLOBIN........................................................................
TB TEST..............................................................................................
VDRL..................................................................................................
HIV TEST...........................................................................................
UPT TEST.........................................................................................
STOOL...............................................................................................
ULCERS.............................................................................................
DIABETIC..........................................................................................
ASTHMATIC......................................................................................
DISABILITIES (If any) ....................................................................
ALLERGIES (If any) ........................................................................
ADDITIONAL INFORMATION.

Eg.Any physical effects or impartment infections, chronic of family disease etc.

1. The student is in good health free from infection diseases and is fit to proceed with studies.
2. The student will be attending treatment for.........................................................................

SIGNATURE..............................................................................................
DESIGNATION................................................................. .......................
STATION.........................................................................................

NOTE: MEDICAL OFFICER.

At the time of Examination, please treat the individual for any ailment you note.

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule ……………** : **0787 886 610** au **0767 941 425.**
- **Makamu Mkuu wa Shule …… 0682 324 009**
- **Mwandamizi Taaluma …………0759 951 823**
- **Mwandamizi Malezi ……………… 0786 839 408**